

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:  
Simu: 2203156/2203158  
Fax: +25522203213  
Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)  
Barua pepe : [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA,**  
3, Barabara ya Rashid Kawawa,  
S.L.P. 5429,  
**12880, DAR ES SALAAM.**  
Tanzania

**14 Agosti, 2020**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**MKUU WA WILAYA ILALA AAPISHWA RASMI LEO**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Abubakar Kunenge amemuapisha Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Ng'wilabuzu Ndwata Ludigija leo tarehe 14 Agosti, 2020 kuwa Mkuu wa Wilaya hiyo kufuatia kuteuliwa kwake na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli tarehe 9 Agosti 2020.

Hafli hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam, Wakuu wa Sehemu na Vitengo na Watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Awali Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam Ngd. Paulo Mshimo Makanza alimkabidhi kiapo Mhe. Ng'wilabuzu na kuapa pia alisoma Ahadi ya Uadilifu kwa Viongozi wa Umma aliyopewa na Katibu Msaidizi Kanda Maalum ya Dar es Salaam Bi. Elizabeth Philipo Komba.

Baada ya hapo aliapishwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Abubakar Kunenge kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala ambapo alipata nafasi ya kuongea pia na kuahidi kutekeleza yote yatakayotolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Aidha aliahidi kuendelea kusimamia vema miradi yote iliyopo katika Wilaya hiyo kama vile miradi ya Maji, Afya, Umeme na Miundombinu ya Barabara.

Akizungumza wakati wa hafli hiyo Mhe. Abubakar Kunenge amempongeza Mkuu huyo wa Wilaya ya Ilala kwa kuteuliwa kwake na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aidha amewataka Wakuu wote wa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam kusimamia suala zima la ukusanyaji wa Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali.

Ameongeza kuwa ili tuweze kukuza kipato katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam ni lazima tuweke mikakati ya kuwavutia wawekezaji aidha kuwepo na mkakati wa kusimamia Mazingira ili kundoa changamoto mbalimbali.

RC Abubakari Kunenge amehimiza uwepo wa Uhusiano mzuri na Chama cha Mapinduzi ambapo ndio tunatekeleza Ilani yake, uwepo wa Amani, utulivu, umoja na mshikamano miongoni mwa wafanyakazi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ili kufanikisha malengo husika.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano  
**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**DAR ES SALAAM**